

# Je, Elimu Maalum ni nini?



Elimu maalum inaweza kumaanisha aina nyingi za usaidizi kwa ajili ya mtoto wako. Inaweza kujumuisha teknolojia, kusoma katika vikundi vidogo, usafiri, tiba ya matamshi na zaidi.

## Elimu maalum hubadilika kutegemea umri wa mtoto wako.

### UMRI 0 - 3

Ikiwa mtoto wako anastahiki, anaweza kujiandikisha katika Mpango wa Mkakati wa Mapema wa Arizona (Arizona Early Intervention Program, AZEIP). AZEIP inatoa uchunguzi na huduma kwa watoto wachanga na wanaoenda dede na familia zao. Unaweza kujaza ombi kwenye [azeip.azdes.gov](http://azeip.azdes.gov).

### UMRI 3 - 5

Mtoto wako anaweza kupokea elimu maalum kwa watoto wachanga ikiwa anastahiki, ikiwemo chekechea bila malipo. Mtoto wako hahitaji kuandikishwa shuleni ili kutathminiwa kwa ajili ya huduma. Wasiliana na wilaya ya shule yako ya karibu kwa maelezo.

### UMRI 5 - 14

Watoto walio na miaka 5 kufikia tarehe 1 Septemba wanaweza kuenda chekechea. Watoto wote wanaoanza chekechea wanachunguzwa hali ya ulemavu. Ikiwa mtoto wako ana zaidi ya miaka 5 na hana rekodi kutoka kwenye shule nyingine, pia atachunguzwa. Ikiwa ulemavu wa mtoto wako haujatambuliwa kwenye uchunguzi huu, unaweza kutuma ombi la maandishi kwenye wilaya ya shule ili kuangalia tena tathmini.

### UMRI 14 - 22

Ingawa wanafunzi wengi huhitimu shule ya upili baada ya miaka 4 baada ya kutimiza matakwa ya shule, baadhi ya wanafunzi walio na ulemavu wanaweza kusalia shuleni hadi wafikishe miaka 22. Wanafunzi walio na zaidi ya miaka 14 pia wanaweza kupokea huduma zinazohusiana na kazi kutoka kwenye mpango wa jimbo wa Marekebisho ya Utaalamu (Vocational Rehabilitation, VR). Huduma hizi ni pamoja na mafunzo na kuunda ujuzi.

**Je, bado una maswali?**  
Tazama miongozo yetu kuhusu *Mipango ya Elimu Iliyobinafsishwa (Individualized Education Programs, IEPs)* na *Kunyimwa Huduma (Denials of Services)* kwa maelezo zaidi.